

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
BARAZA LA MITHANI LA TANZANIA
MTIHANI WA UALIMU DARAJA LA A**

636

TEHAMA

Muda: Saa 3

Mwaka : 2021

Maelekezo

1. Karatasi hii ina sehemu A na B zenye jumla ya maswali **kumi na sita (16)**.
2. Jibu maswali **yote** katika sehemu A na maswali **manne (4)** kutoka sehemu B.
3. Sehemu A ina alama **arobaini (40)** na sehemu B ina alama **sitini (60)**.
4. Simu za mkononi na vitu vyote visivyoruhusiwa **havitakiwi** ndani ya chumba cha mtihani.
5. Andika **Namba yako ya Mtihani** katika kila ukurasa wa kijitabu chako cha kujibia.



SEHEMU A (Alama 40)

Jibu maswali **yote** katika sehemu hii.

1. Elezea kwa kifupi hatua tano anazopaswa kufuata mwalimu wakati wa kutumia televisheni kufundishia mada ya kusikiliza kwa usahihi habari iliyosemwa.
2. Ainisha changamoto nne zinazoweza kumfanya mwanafunzi kuhitaji ushauri nasaha.
3. Elezea kwa kifupi dhana zifuatazo kama zinavyotumika katika uunganishaji wa mtandao wa kompyuta:
(a) Seva (b) Routa
(c) Modem (d) Swichi mtandao
4. Fafanua kwa kifupi changamoto nne anazoweza kupata mwalimu iwapo atakabidhiwa kufundisha somo la TEHAMA bila muhtasari.
5. Bainisha njia nne zinazoweza kumsaidia mwalimu wa somo la TEHAMA kupata zana.
6. Eleza kwa kifupi faida nne za uwepo wa alama zinazoashiria hatari barabarani.
7. Fafanua misingi minne anayotakiwa kuzingatia mwalimu wakati wa kutunga maswali ya kuoanisha.
8. Bainisha hatua nne anazopaswa kufuata mwanafunzi wakati wa kutumia program andishi ili kuchapa nyaraka.
9. Fafanua kwa kifupi faida nne za matumizi ya TEHAMA katika mawasilino.
10. Eleza kwa kifupi mambo manne yanayotakiwa kuzingatiwa ili kuweza kutunga maswali mazuri ya kuchagua kwa ajili ya upimaji katika somo la TEHAMA.

SEHEMU B (Alama 60)

Jibu maswali **manne (4)** kutoka sehemu hii.

11. Jadili mambo matano yanayoweza kuonesha kuwa, msingi wa usawa wa kijinsia hauzingatiwi wakati wa kufundisha na kujifunza somo la TEHAMA.
12. Kwa kutoa hoja tano, jadili umuhimu wa vituo vya ushauri nasaha kwa vijana na wanafunzi wa shule za msingi.

13. "Utunzi wa zana nzuri za upimaji huhitaji maandalizi mazuri hasa ya jedwali la utahini." Thibitisha usemi huu kwa kuonesha hatua tano muhimu zinazotakiwa kufuatwa wakati wa utayarishaji wa jedwali la utahini.
14. Changanua njia tano anazoweza kutumia mwalimu ili kuweka darasa katika hali ya utulivu.
15. Kwa kutumia hoja tano, eleza kwa kina umuhimu wa kufanya uchambuzi wa muhtasari wa somo la TEHAMA kama maandalizi muhimu ya ufundishaji na ujifunzaji.
16. Jadili misingi mitano anayotakiwa kuzingatia mwalimu wa somo la TEHAMA katika kubuni na kutengeneza zana za kufundishia na kujifunzia.